**Vidokezo:**
**Maelezo Kuhusu Darfur kwa Makamanda na Wapiganaji wa Jeshi la Ulinzi la Tanzania – JWTZ**
**(Jumanne, 31 Machi, 2009)**

1. **Maelezo mafupi ya jiografia, historia na mazingira ya siasa huko Darfur, Magharibi ya Sudan.**

   - Darfur ni Mkoa wenye wilaya tatu (3) [Kaskazini, Kusini na Magharibi]
   - Eneo: Kilomita za mraba 1809 au maili za mraba 186,000 (Ni sawa na eneo la Ufaransa].

2. **Makabila na Dini**

   - Wananchi (2006): Kusini watu 2,890,000, Magharibi watu 1, 007,000; na Kaskazini watu 158,000
   - Makabila : Massalif, Zaggana, Baggara, Tarjem, Mahria, Murle Fur, Abbala n.k.
   - Kilimo: Hulima mtama na kufuga katika maeneno yanayolimika. Mvua: 700mm kwa mwaka.
   - Makao Makuu: El- Fasher

3. **Kiini cha Matatizo:**

   - Darfur – kwa Kiarabu: Himaya ya Wafu
   - Ilijulikana tangu, 10,000 B.C
   - 1875 Darfur ilivamiwa na Wamisri (Mtawala: Abdallah ibin Mohamed).
   - 1899 Majeshi ya Misri na Waingereza walimg'oa Abdallah ibin Mohamed (walimuweka Ali Dinar kuwa Sultan)

- 1916 Anglo/Sudan waliitwaa Darfur kwa hofu isiende kwa Waturuki

**Angalizo:**
Serikali zote hazikujali hali ya Wadarfur

- Sudan ilipata Uhuru toka Waingereza, Wa-Darfur walisahauliwa zaidi
    - Sera za Uarabu kwanza (za Libya)
    - Vita vya 1955 – 1972 na 1983/2005

- 1980 Baalaa la njaa lilizidisha matatizo na magomvi ya "maeneo na haki za maji".

- Wananchi walichoka kuonewa, kunyanyaswa, na hatimaye walichukuwa hatua ya kuchukuwa mtutu wa bunduki (2003). SLM/A na JEM

**4. Matokeo:**

- Mapigano yalianza 2003
- Watu waliohufa kwa vita na njaa ni kati ya 200,000 na 300,000
- Wananchi waliosambaratishwa ndani ya nchi ni milioni 2 – 2.5 (IDPs)
- Wananchi 200,000 walikimbilia Chad (Wakimbizi)

**5. Wahasimu:**
- Serikali ya Sudani (Ikiongozwa na NCP)
- Waasi wa Darfur
    - Sudan Liberation Movement/Army, SLM/A
    - Justice and Equality Movement (JEM)

**6. Maeneo Mengine ya Migogoro (Sudan)**

- Sudani ya Kusini - CPA 9 January, 2005
    - Serikali ya Sudan/SPLM: 1983
    - Mgogoro wa raslimali, madaraka na suala la dini na kujitawala
    - Wananchi 2 millioni wamekufa, 4m wamesambaratika

- Chini ya IGAD:: SPLM na Sudan walikubaliana:
    - Protockali ya Machakos: 20/07/2002 (Utawala)
    - Protokali Usalama: Naivasha 25/09/2003
    - Protokali kugawana Raslimali: Naivasha 07/01/2004
    - Protokali ya Madaraka: Naivasha 26/05/2004
    - Protokali ya Kordofan / Milima ya Nuba: Naivasha 26/5/2004
    - Protokali ya Abyie: Naivasha 26/05/2004

- Kordofan:
    - Jimbo lililoundwa na CPA (2005)
    - Makabila ya hapo: Musseriya, Hawazina na Nuba
    - DDR haijafanyiwa kazi kama CPA ipasavyo
    - 2% ya mapato hayajalipwa ipasavyo
    - Kuundwa chombo cha kuratibu na kutekeleza

7. **Juhudi za Kutatua Mgogoro:**

- Makubaliano ya N'djamena
    - Saini tarehe 08/04/2004 N'djamena

- Walioweka saini: GOS, SLM/A na JEM
    - Ibara (articles) 11 zenye maudhui yafuatayo:-
      (a) Kupanga na kuthibitisha utekelezaji
      (b) Kuelekeza barabara za wapiganaji
      (c) Kufukua mabomu
      (d) Kupokea na kuchambua ukiukwaji wa makubaliano
      (e) Wahusika kuwajibika kutoa taarifa
      (f) Kwenda popote Darfur
      (g) Kuelewa wapiganaji wapo wapi, kuthibitisha kuzimwa kwa Janjaweed.

- Matatizo ya Utekelezaji (HCFA)
    - HCFA: nafasi ya kujua nguvu za dini
    - Wapiganaji walichelewesha ukaguzi wa matukio
    - Posho kugharamia mapambano

- AMIS: (2004)
    - AUPSC kuidhinisha askari 300 Darfur
    - Juni 2004:- Ujenzi wa Makambi
    - Kuongeza askari 2941, na Poliisi 815
    - Expanded AMIS: askari 6,171 na askari (raia) 1560 kutoka:-
        - Nigeira,
        - Rwanda
        - South Africa
        - Senegal
        - Kenya na
        - Gambia

- AMIS: Matatizo ya Utekelezaji
    - Matatizo ya lugha
    - Kutegemea mno misaada ya nje (vifaa na fedha)
    - AMIS intelligence ilikuwa na mapungufu
    - Oktoba, 2005 – Wanaijeria wawili waliuawa
    - AMIS ilipoteza jumla ya askari 59.

**Angalizo:**

(a) AU ilijihusisha kutoka mwanzo katika suala la Darfur kwa kupeleka sakari – Walinzi wa Amani

(b) AU nguzo ya amani na maendeleo Afrika

(c) Mtatuzi wa matatizo ya Afrika (Burundi, Somalia, Darfur)

(d) Kuratibu misaada

**8. Mazungumzo ya Amani: Abuja (Juni 2005 – May 2006)**

- Misingi ya mazungumzo:
    - Sudani ni moja – hakuna kugawanywa
    - Ufumbuzi ni wa siasa siyo kwa mtutu wa bunduki
    - Majadiliano yanawahusu watu wote
    - Kusiwekwe ratiba ya kumaliza mazungumzo
    - DOP - 5 Julai, 2005

- Yaliyojadiliwa (Duru ya 5 – 7)

(a) Power Sharing: Madaraka
- Haki za kiraia
- Nguzo tatu za uongozi wa serikali zidumishwe
- Kuheshimu haki za binadamu
- Kugawana madaraka ni msingi wa umoja
- Uchaguzi uliowazi, wa haki kwa ngazi zote
- Vyombo vya seriklai viwakilishe wananchi wote
- Utamaduni kuendelezwa,
- Wanawake washirikishwe kikamilifu
- Utawala Darfur – TDRA (Mikoa 3)
- Mipaka ya Darfur iwe ya 01/01/1956

(b) Wealth Sharing (Raslimali)

- Haki sawa katika maendeleo
- Ushiriki sawa katika kuandaa sera za maendeleo
- Uwakilishi katika vyombo vyote vya kugawa raslimali
- Kushughulikia maeneo yaliyoathirika na vita
- Kuwashirikisha wanawake
- Kutambua "hawakeer" na matumizi yake
- Kurekebisha uwiano wa sheria za kodi (Serikali Kuu/ Darfur)
- Kufidia Wadarfur (Dola, 1000 kila IDP)
- Kuundwa kkwa Tume ya Ardhi
- Kuundwa kwa Darfur R.R.C

(c) Security Arrangements (Usalama)
- Umuhimu wa C.C.F
- Kuzingatia makubaliano ya:-

| | |
|---|---|
| (a) N'djamena | April 2004 |
| (b) Addis Ababa | May 2004 |
| (c) Abuja Protocol | November, 2004 |
| (d) DOP | July 2005 |

- <u>Lengo la C.C.F.A ni:-</u>

  (a) Kuzuia mapigano
  (b) Raia hawadhulumiwi au kuhamishwa
  (c) Misaada inawafikia walengwa
  (d) Kurahisisha kurudi kwa IDP's kwao
  (e) Ushirikiano mzuri na AMIS
  (f) Kuacha mapigano na kuyapanga upya majeshi
  (g) Misaada isiyo ya kijeshi kwa Wapiganaji

**Angalizo:**

Madai ya wapiganaji yalijumlisha yale majimbo matatu - Kaskazini, Kusini na Magharibi yawe Jimbo moja tu!

- <u>DDDC (Dialogue)</u>
  - Maelezo: Mkutano wa Wa-Darfur wote ili kujadili hatima ya Darfur
    - (a) Utengamano
    - (b) Kuepuka mfarakano
    - (c) Kutatua matatizo yaliyopo
    - (d) Kujenga nchi.
  - Kuitangaza DPA
  - Kuimarisha amani
  - Kusawazisha masuala ya usalama, kuchambua vyanzo vya matatizo
  - Kushirikisha umma na Darfur kwa uwakilishi wnaokubalika

## 9. Makubaliano ya Darfur (DPA)

- Yaliwekwa saini tarehe 5 May 2006
- Yaliwekwa saini na:-
  - Serikali ya Sudani - Dr. Mazjoub El Khalifa
  - SLM/Mini - Mini Minawi

- <u>Walikataa kuweka saini</u>
  - SLM/Abdul Wahid - Abdul Wahid
  - J E M - Dr. Ibrahim Khalil

- Mafanikio ya DPA
    - Yalirekodi mapatano yote (siasa, uchumi, ulinzi n.k.)
    - Yaliandaa utaratibu wa Mapato
    - Yalishirikisha Wadau mbalimbali
    - Yaliandaa mafunzo kabla ya vikao
    - Yaliainisha maeneo ya kutekelezwa na Wadau mbalimbali
    - Yalipania kuwashirikisha wanawake ambao wanasahaulika katika jamii ya Sudani.

- Mapungufu ya DPA
    - Kudhani kwamba kuna kikosi cha kusimama
        (a) Kujua wapiganaji wapo wapi
        (b) Kusimamia upokonyaji wa silaha
        (c) Kusimamiisha mapigano
        (d) Ulinzi wa IDPs
        (e) Ulinzi wa misaada ya kibinadamu
        (f) Jumuia ya Kimataifa kushindwa kushinikiza
        (g) Kutengua na kuunganisha majeshi

**10. Majukumu ya Nchi za Kanda**

- Nchi husika:- Eritrea, Misri na Chad

**Angalizo:**
Sudan na Chad wamenshutumiana na kuhasimiana tangu 23/12/2005

- Vikao vya nchi za Kanda
    - Kuendeleza juhudi za usuluhishi
    - Kuunganisha juhudi za upatanishi chini ya AU
    - Kuzihimiza Serikali za Chad na Sudan kupatana
    - Kuitaka JEM isiwe kizingo kwa vyama vingine
    - Kumtaka Abdul Wahid ajiunge katika mazungumzo ya Amani Darfur

- Mazungumzo yalifanyika:
    - Tripoli
    - Eritrea
    - Misri (Mara 2)

**11. Wadau wa Kimataifa**

- Umoja wa mataifa (UN)
- Marekani
- Uingereza
- Uholanzi
- Ufaransa
- Umoja wa Ulaya (EU)
- Kanada
- Norwei
- Ujerumani
- Italia

**Angalizo:**

Nchi za Japan na Uchina ziliongezeka baada ya kuweka saini DPA.

- Walikutana Geneva 18 Machi 2008; na Geneva 5 Juni, 2008

- Misaada waliyotoa
    - Baadhi ya misaada iliyotolewa:-
        - Uingereza - Magari na fedha
        - Kanada - APCs 35, Helkopta 18
        - Arab League - Fedha
        - NATO - Kusafirisho vikosi n.k

**12. Mchango wa Nigeria**

- Abasanjo - Kusimamia mazungumzo
- Nigeria kuwa mwenyeji wa Mazungumzo (Abuja)
- Kutoa wataalamu wa kusaidia mazungumzo

**13. Maendeleo baada ya DPA**

- Abuja kulikuwa na SLM/A na JEM
- SLM/A iligawanyika:-
    - SLM/Mini Minawi
    - SLM/Abdul Wahid

**Angalizo:**

Mpasuko wa SLM/A ulitokea Haskanita (2005). Abdul Wahid ni Mwenyekiti wa SLM/A (Asilia) na Mini Minawi alikuwa Katibu Mkuu wake.

- Mpasuko uliendelea kufikia vyama 20 miongoni mwa vyama maarufu ni pamoja na:-

SLM/A Mini - Mini Minawi
JEM - Dr. Khalil Ibrahim
SLM/Abdul Wahid - Abdul Wahid Nour
SLM/A Freewill - Dr. Adurahman Moussa
URF (United Resistance Front- Bakari Abu Garda
SLM/Unity - Abdallah Yahya
SLM/Peace - Ibrahim Maibo
JEM/Peace wing - Abdurisha Abdurahman
SLA/AS - Abul Shafi
JEM/Collective - Bahar Idris Abu Garda
JEM /AZRA - Idriss Ibrahim Arzaq

**14. Mkutano: AU/UN Addis Ababa**

**Angalizo:**

Baraza la Usalama (UN)

- Walipitisha Azimio No. 1769 la 31/07/2007
- Kuunda hybrid – UNAMID – Darfur
- Lengo:
  - Kutekeleza DPA
  - Kulinda wananchi wa Darfur
  - Kuwalinda wafanyakazi wa UN
  - Kukabiliana na chokochoko

- High Level consultation: 16 November, 2006

- Waliohudhuria:
  - Dr. Kofi Annan - Katibu Mkuu UN
  - Dr. Oumar Konare - Mwenyekiti AU
  - Dr. Salim Ahmed Salim - Mwakilishi Mkuu AU Msuluhishi
  - Bw. Jan Eliasson - Mwakilishi Mkuu UN
  - Wajumbe 5 wa Security Council
  - Serikali ya Sudan

- Kuimarisha kusitisha mapigano
    - Wahusika washirikiane na AMIS
    - Jumuia ya Kimataifa ichukue hatua dhidi ya wale watakaojitenga na mkono wa sias
    - Serikali ya Sudan ishirikiane

## 15. Matokeo ya Juhudi Shirikishi

- Juhudi za mashauriano
- Kuleta mshikamano miongoni mwa wapiganaji
- Kukutana na wapiganaji (Jabel Mara, Wadd Sira)
- Kuonana na viongozi wa Serikali
- Kuonana na viongozi wa vyama vya upinzani
- Kuonana na vyama vya kiraia (wasomi, wanawake, viongozi wa dini, viongozi wa makabila nk).
- Mabalozi wa Afrika waliopo Khartoum
- Viongozi wan chi za Kanda (Eritrea, Misri, Libya na Chad).

➢ Yaliyojitokeza:

- JEM kujifanya mwakilishi pekee
- SLM/Abdul Wahid - Kuweka masharti:
    - (a) Janjaweed kukamatwa
    - (b) Fidia (USD 1000) kwa Wakimbizi na IDPs
- Ushirikiano na SPLM na serikali ya Sudan ya Kusini – Kutumia uzoefu wao
- Jumuia ya Kimataifa kujitokeza zaidi (Wajumbe wa UN Security Council)

## 16. Uteuzi wa Mwakilish Darfur

➢ Kwa nini?

- Kuwa karibu na hali halisi
- Wasuluhishi wawili kwa pamoja hawawezi kuendesha usuluhisho
- Kupata muda zaidi wa kushughulikia matatizo
- Kuwa na chombo kimoja kiutendaji

- Nani walipendekeza?
    - Mh. Dr. Salim Ahmed Salim (AU)
    - Bw. Jan Eliasson (UN)
- Nani alipendekezwa
    - Bwana Djibril Bassole
- Cheo: Joint Mediation Chief

**17. Hali ya usalama Darfur**

- Vyama vya Upinzani (wapiganaji)
    - JEM in nguvu zaidi kiusalama
    - SLM/ ina nguvu hususan miongoni mwa makambi (IDPs)
    - UNAMID haiwezi kuhudumia mipaka yote
    - Upatikanaji wa helikopta bado ni utata
    - Janjaweed bado wanaendelea kubugudhi wananchi
    - Serikali haina mpango wa kuwakabili Janjaweed

**18. Taathira: Hati ya kumkamata Al Bashir**

- Mtafaruku wa fikra
    - Serikali ya Sudan si Mwanachama wa ICC
    - Serikali ya Sudan ni Mwanachama wa UN
    - Maendeleo ya amani yanavurugwa

- Matokeo
    - Mashirika 13 ya Kimataifa yametimuliwa
    - Mapigano bado yanaendelea
    - Janjaweed wanaendeleza harakati zao
    - Serikali kushindwa kutekeleza DPA
    - Misaada kwa watu wa Darfur kupungua

**19. Matarajio**

- Juhudi za kutafuta amani sharti ziendelee
    - Nchi za jirani na Sudan
    - Jumuia ya Kimataifa zitekeleze miadi
    - Wa-darfur waungane
    - Sudan izibe pengo la waliofukuzwa

- <u>Umoja wa Mataifa</u>
  - Uahirishe kukamatwa Al Bashir
  - Jumuia ya Kimataifa isiibwage Darfur

**20. Sudan ni Muhimu**

- Inapakana na nchi nane za Afrika (Chad, Kenya, Uganda, Misri, Libya, DRC, Ethiopia, Eritrea na Central African Republic)
- Ni nchi kubwa kuliko zote Afrika
- Inahitaji msaada wa Afrika yenyewe pia.